JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

015 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda : Saa 3 **Mwaka: 2024**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **mawili (2)** katika sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina **alama thelathini (30)**.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 401015 100019

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Bainisha njia ya mawasiliano kati ya Allah (S.W) na waja wake ambayo inaendelea kutumika hadi zama hizi ingawa hakuna tena Mitume na Manabii.

A Kupata Ilham katika mambo mbalimbali
B Kuongea na Allah (S.W) nyuma ya pazia
C Kupokea maagizo kutoka kwa Malaika
D Kumuota Mtume Muhammad (S.A.W)
E Kupokea kurasa zenye ujumbe toka mbinguni

(ii) Nini kinasababisha watu ambao hawaamini Mwenyezi Mungu wanapopata matatizo au misukosuko ya maisha wanamkumbuka Mungu muumba?

A Msukumo wa kimazingira
B Ishara wanazoziona katika nafsi zao
C Kuwepo kwa Wahyi
D Ishara ya kuwepo kwa Fitrah
E Dalili katika vipaji vya wanadamu

(iii) Ishara gani inaonesha kueleweka vibaya kwa dhana ya Dini miongoni mwa Waislamu katika jamii ya sasa?

A Kuyagawa maisha katika misingi ya maisha ya Dini na Dunia
B Viongozi na waumini wa Kiislamu kujadili mambo ya kisiasa
C Kufundisha somo la Elimu ya Dini katika shule za sekondari
D Kujifunza au kusomesha mafundisho ya Dini kwa Kiswahili
E Kutekeleza ibada katika mavazi mengine yasiyokuwa kanzu

(iv) Kwa nini dhana ya Ibada katika Uislamu kwa ujumla haifungamani na wakati mahususi?

A Katika Uislamu kila mtu ana uhuru wake.
B Kiislamu ni haramu kuabudu baadhi ya nyakati.
C Wakati huwa unabadilika kutokana na misimu.
D Ingekuwa vigumu kutekelezwa na waumini.
E Katika Uislamu kila jambo jema ni ibada.

(v) Kaburi la Muislamu litafukuliwa na maiti kuzikwa upya endapo hakufanyiwa mambo gani?

A Hakuoshwa, hakukafiniwa na kuvikwa sanda
B Hakukafiniwa na hakuvikwa sanda nyeupe
C Hakuvikwa sanda na hakusaliwa na wengi
D Hakuoshwa, hakuvikwa sanda na hakusaliwa
E Hakukafiniwa, hakuoshwa na hakusafishwa

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

(vi) Utukufu wa mji wa Makkah umetokana na jambo gani la kihistoria?

A Kuwepo kwa neema ya matunda ingawa ni jangwa.
B Kuwepo kwa Al Qaabah kama nyumba ya ibada
C Kuzaliwa kwa bwana Mtume (S.A.W) ndani yake
D Kuanzishwa kwake na Nabii Ibrahim na Ismail
E Kufikiwa na wageni wengi kwa ajili ya kufanya ibada

(vii) Katika maisha ya Nabii Adam (A.S), jambo gani linaonesha aliandaliwa kuwa Khalifa?

A Kuwashinda Malaika kielimu.
B Kuumbiwa kila kitu duniani.
C Kufanyiwa uadui na Ibilis.
D Kupewa elimu zote muhimu.
E Kuishi peponi na mke wake.

(viii) Bibi Aisha (R.A) alipoulizwa juu ya tabia ya Mtume (S.A.W) alijibu kuwa *"tabia yake ni Qur'an"*. Majibu hayo yanatoa mafundisho gani?

A Qur'an ni maneno ya Mtume (S.A.W)
B Mtume (S.A.W) ni sehemu ya Qur'an
C Qur'an ni sehemu ya Mtume (S.A.W)
D Mtume (S.A.W) ni kielelezo cha Qur'an
E Qur'an ni tawasifu ya Mtume (S.A.W)

(ix) Kwa mujibu wa historia ya Qur'an, ni sura gani ilianza kuteremshwa kwa ukamilifu?

A Sratul - Faatihah
B Suratul - Alaq
C Suratul - Muzammil
D Suratul - Mudathir
E Suratul - Nasr

(x) Ikiwa mkulima amevuna mahindi kilo1,335 katika shamba lake la kilimo cha umwagiliaji, ni kiasi gani cha Zakat atapaswa kutoa kwa mujibu wa Uislamu?

A 33.3 kg
B 666 kg
C 66.6 kg
D 99.9 kg
E 133.2 kg

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

2. Oanisha maelezo kuhusu aina za maji yanayofaa kujitwaharisha katika **Orodha A** na majina/sifa zake katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi chini ya namba ya kirumi katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		Orodha B	
(i)	Sifa ya jumla ya maji twahara ambayo mtu anaruhusiwa kuyatumia kwa ajili ya maandalizi ya ibada.	A	Maji machache
(ii)	Maji yaliyokusanywa katika chombo au yaliyojikusanya katika ardhi yakiwa chini ya lita 240.	B	Dhiraa
(iii)	Maji ya aina zote katika vyanzo vyake na yaliyobaki katika asili yake.	C	Maji mutlak
(iv)	Maji yaliyonywewa na binadamu au mnyama halali na kubakishwa.	D	Qullatain
(v)	Kipimo mahususi cha maji ambacho ni sawa na ujazo wa lita 240.	E	Maji makombo
(vi)	Maji yaliyokusanywa katika chombo au kujikusanya katika ardhi na kufikia ujazo wa lita 240 au zaidi.	F	Maji mengi
		G	Maji matamu
		H	Maji safi

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Orodhesha faida sita za kijamii anazozipata mwanadamu kutokana na kumuamini Mwenyezi Mungu (S.W).

4. Mambo gani yanapaswa kuzingatiwa na mwanamke anayetarajia kufunga ndoa ya Kiislamu? Taja mambo sita.

5. (a) Bainisha mikataba mitatu ya amani aliyofunga Mtume (S.A.W) mwanzoni mwa Dola ya Kiislamu.

   (b) Toa mafunzo matatu yanayopatikana kutokana na kufungwa mikataba hiyo.

6. (a) Mambo ya halali katika Uislamu yamegawanywa katika hukumu tatu. Bainisha hukumu hizo.

   (b) Toa mifano miwili kwa kila hukumu uliyoitaja katika (a).

7. Ainisha haki sita za binadamu kama zilivyobainishwa katika Uislamu.

8. Michakato ya kupatikana Makhalifah watatu wa mwanzo baada ya kufariki Mtume (S.A.W) ni ishara kuwa Uislamu ni chuo cha mifumo bora ya kiuchaguzi na upatikanaji wa wasimamizi wa umma.

   (a) Thibitisha kauli hiyo kwa kuonesha njia tatu zilizotumika kuwapata Makhalifah hao.

   (b) Taja njia zingine tatu zinazokubalika katika Uislamu ili kuwapata viongozi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii.

9. Bainisha faida tano za kijamii zitazopatikana endapo ibada ya Zakat itatekelezwa.

10. Onesha hekima tano za kushushwa Qur'an kwa lugha ya Kiarabu.

11. Bainisha nafasi ya *Sanad* (Isnad), *Matini* (Matn) na *Rawi* katika kuthibitisha usahihi wa Hadithi za Mtume (S.A.W).

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner